4.0 KISWAHILI (102)

MANYAM FRANCHISE
Discover|Learn|Apply

4.1 MATOKEO YA MTIHANI WA SOMO LA KISWAHILI:

Jedwali hili linaonyesha matokeo ya mtihani wa somo la Kiswahili katika muda wa miaka minne (2006 hadi 2009)

Jedwali 4: Matokeo ya Somo la Kiswahili (2006 – 2009)

Mwaka	Karatasi	Watahiniwa	Alama ya Juu	Alama ya Wastani	Alama ya Tanganisho
2006	1		40	15.31	7.68
	2		80	40.60	11.80
	3		80	48.48	14.63
	Jumla	**241272**	**200**	**104.39**	**29.00**
2007	1		40	15.80	6.42
	2		80	32.22	11.91
	3		80	43.49	13.12
	Jumla	**272905**	**200**	**91.51**	**27.00**
2008	**1**		40	14.20	7.18
	2		80	29.18	11.43
	3		80	31.17	13.64
	Jumla	**304314**	**200**	**74.55**	**32.25**
2009	**1**	**335118**	40	15.40	6.93
	2	**335296**	80	29.03	11.96
	3	**335167**	80	32.72	13.11
	Jumla		**200**	**77.15**	**32.00**

Jedwali hili laonyesha kuwa kwa ujumla:

4.1.1 Alama ya wastani ya karatasi ya 1(102/1) ya mwaka wa 2009 imeimarika ikilinganishwa na mwaka wa 2008

4.1.2 Matokeo ya karatasi ya pili (102/2) ya mwaka wa 2009 yameshuka kidogo yakilinganishwa na yale ya mwaka wa 2008.

4.1.3 Matokeo ya karatasi ya tatu (102/3) ya mwaka wa 2009 yameimarika kutoka alama ya wastani 31.17 mwaka wa 2008 hadi 32.72 mwaka wa 2009.

4.1.4 Matokeo ya Kiswahili kwa jumla katika mwaka wa 2009 yameimarika. Alama ya wastani ya Kiswahili kama somo ni 77.15 yakilinganishwa na mwaka wa 2008 ambapo alama hii ilikuwa 74.55(ongezeko la 2.6)

4.1.5 Alama ya tanganisho inaonyesha kuwa kuna baadhi ya watahiniwa ambao waliweza kujipatia alama nyingi zaidi ya alama ya wastani mwaka wa 2009.

4.2 INSHA (102/1)

Jedwali 5: Matokeo ya Karatasi ya kwanza ya miaka ya 2006 – 2009.

Mwaka	2006	2007	2008	2009
Alama ya Wastani	15.31	15.80	14.20	15.40
Alama ya Tanganisho	7.68	6.42	7.18	6.93

Powered By: www.manyamfranchise.com

Jedwali hili laonyesha kwamba kwa miaka minne mfululizo (2006-2009), matokeo ya karatasi ya 102/1 yamekuwa mabaya na kwamba watahiniwa wengi hawajaweza kujipatia alama zaidi ya nusu ya alama zote ambazo zinaweza kutuzwa ambazo ni 40 ingawaje alama ya wastani imeimarika mwaka wa 2009 kwa kiasi cha **1.2** ikilinganishwa na mwaka wa 2008.

Tutachanganua swali la kwanza ambalo lilikuwa la **lazima** na ambalo halikufanywa vizuri, na vilevile swali la **tatu** ambalo lilijaribiwa na watahiniwa wachache zaidi ya maswali mengine na hata wachache hao walitatizika pakubwa, huku wengi wao wakipotoka.

Swali la 1

Insha ya **lazima.**

Umealikwa kitongojini mwenu kama mgeni wa heshima katika hafla ya kuzindua kundi la wasanii wa Kikwetu. Andika hotuba utakayotoa ya kuonyesha umuhimu wa sanaa na michezo.

Watahiniwa walikosa alama kwa sababu wengi hawakuilenga hadhira iliyotarajiwa yaani kundi la Kikwetu. Kadhalika, walishughulikia kwa ujumla kuhusu michezo ya riadha,kandanda na kadhalika (michezo ya uwanjani) badala ya michezo ya kisanaa (ya jukwaani) kama vile drama, nyimbo, ukariri wa mashairi na matumizi mengine ya vipawa katika sanaa ya uigizaji.

*Tafadhali tazama mwongozo ulioambatanishwa katika ripoti hii ili uone jinsi insha hii ya hotuba ilivyostahili kuandikwa.

Swali la Tatu

Samaki huanza kuoza kichwani.

Hili lilikuwa swali la methali.Watahiniwa walipotoka katika kutafsiri maana ya methali hivyo basi wakapotoka katika hoja walizoshughulikia.

Aidha, watahiniwa wengi hawakulijaribu swali hili kabisa.

Mtahiniwa alitarajiwa aandike insha juu ya kisa kimoja kinachodhihirisha kuwa asasi yoyote ya kijamii ambayo imepotoka au ina kasoro/dosari/ila/udhaifu (uozo),huanzia kwa viongozi wake. Kwa mfano watoto wakikosa maadili, kuna uwezekano mkubwa kuwa wazazi ndio waliotangulia kuyakosa maadili hayo.

4.3 MAPENDEKEZO:

- Walimu wazidi kuwapa wanafunzi mazoezi zaidi katika uandishi wa kiuamilifu.
- Walimu watumie silabasi za K.I.E. na K.N.E.C. katika ufundishaji wao.
- Wanafunzi wahimizwe kusoma magazeti na kujifahamisha na matukio ya kila siku katika jamii na mazingira yao-kitaifa na pia kimataifa; ilmuradi waweze kuyashughulikia maswali yanayohusu maswala ibuka iwapo yatatahiniwa. Wasijikite katika maswala yaliyo vitabuni pekee.

4.4 LUGHA (102/2)

Jedwali 6: Matokeo ya Karatasi ya pili (102/2) ya miaka ya 2006 hadi 2009.

Mwaka	2006	2007	2008	2009
Alama ya Wastani	40.60	32.22	29.18	29.03
Alama ya Tanganisho	11.80	11.91	11.43	11.96

Matokeo ya karatasi ya 102/2 yameshuka mwaka wa 2009. Matokeo haya ndiyo ya chini zaidi katika kipindi cha miaka minne.
Maswali ya ufahamu na ufupisho/muhtasari ndiyo yaliyowatatiza watahiniwa.

Powered By: www.manyamfranchise.com

Tutayachanganua hapa.

Swali la 1

UFAHAMU

Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.

Wanasaikolojia wanabainisha kati ya sehemu mbili kuu katika akili ya binadamu: ung'amuzi na ung'amuzibwete. Ung'amuzi ni sehemu ya ubongo ambayo kimsingi hupanua na kudadavua yanayotendeka hususan mchana. Ung'amuzibwete ni kibinimethali chake; hufanya kazi wakati binadamu anapoteuazwa na usingizi. Baadhi ya mambo anayoshuhudia binadamu mchana yanaingia kwenye ung'amuzibwete wake na kutokeza katika ndoto zake usiku.

Kwa mujibu wa mawazo ya Sigmund Freud, mwanasaikolojia wa jadi anayechukuliwa na wengi kama mwasisi wa taaluma ya saikolojia, mambo yanayopatikana katika ung'amuzibwete yana sifa hasi. Freud alidahili kuwa binadamu huyaficha na kuyabania kwenye ung'amuzibwete mambo ambayo hawezi kuyasema kadamnasi. Alieleza kuwa matamanio yasiyokubalika, makatazo ya jamii, fikra na kauli zilizoharamishwa na miko ya kijamii hubanwa katika ung'amuzibwete. Shehena hiyo ndiyo inayochipuza kwa njia ya ishara za ndoto, mitelezo ya kauli, yaani maneno au kauli zinazotutoka bila wenyewe kukusudia, ishara na lugha ya kitamathali katika uandishi wa kibunifu na kadhalika.

Ung'amuzibwete una uwezo mk..5wa wa kuathiri matendo ya binadamu. Huu ndio msingi unaowafanya wanasaikolojia wengi, akiwepo Freud, kusema kuwa tajriba ya mtoto inaweza kufichwa kwenye sehemu hiyo na hatimaye kuishia kutokeza katika utu uzima wake. Kwa kuwa tunapoingiliana na binadamu wenzetu kila siku tunayang'amua tuyafanyayo, ung'amuzi unaotuwezesha kutambua jema na ovu unatawala. Ung'amuzibwete unapotawala binadamu wenzetu watashindwa kutuelewa. Hii ndiyo hali anayokuwa nayo mwendawazimu. Ung'amuzibwete wake hutawala. Sisi tunaotawaliwa na ung'amuzi tunashindwa kumwelewa; naye bila shaka anashindwa kutuelewa.

Carl Gustav Jung, aliyewahi kuwa mwanafunzi wa Freud, aliupinga mwelekeo wa Freud wa kuuangalia ung'amuzibwete kama jaa la mawazo mabaya, matamanio, nia, fikira tuli na dhana ambazo ni hasi. Jung alizuka na dhana mbili muhimu: Ung'amuzibwete wa kibinafsi na ung'amuzibwete jumuishi. Alisema mambo, fikra na uzoefu wowote mbaya unaomuhusu mtu binafsi hupatikana katika ung'amuzibwete wa kibinafsi. Dhana ya ung'amuzibwete jumuishi aliitumia kuelezea sehemu ya akili ya binadamu ambayo inamfanya ayatende matendo fulani kama binadamu wenzake licha ya tofauti zao kiwakati na kijiografia. Kwa mfano, binadamu wengi wana sherehe za kuzaliwa mtoto, kuoza, ibada au mviga unaohusiana na kifo licha ya tofauti zao. Jung alisema kuwa kinachochochea hali hii ni urithi fulani wa kila mwanadamu. Urithi huo unapatikana katika ung'amuzibwete jumuishi.

Upo mwafikiano kati ya wataalamu hawa wawili kuwa ung'amuzibwete una uwezo wa kuathiri ung'amuzi na matendo ya binadamu ya king'amuzi. Wanasaikolojia wanashikilia kuwa binadamu hawezi kukamilika bila kuzihusisha sehemu zote mbili kwa sababu zinaathiriana.

Kwa ujumla, maswali ya kifungu yalihitaji mtahiniwa asome, aelewe na kuchanganua, kusanisi, kutafsiri, kutathmini na kutumia maudhui katika kifungu kujibu maswali.

Watahiniwa wengi waliinua majibu moja kwa moja kutoka kwa kifungu, jambo ambalo linafanya majibu yasiwe na mtiririko unaoridhisha.

Watahiniwa pia walikosa alama katika swali hili kwa sababu wengi hawakuwa na stadi ya kujieleza vizuri na hivyo wakafanya makosa mengi ya sarufi na tahajia.

Swali la 1 (a)

(a) Kwa nini ung'amuzibwete unaelezwa kama kinyume cha ung'amuzi?

Majibu

Ung'amuzibwete hufanya kazi mtu anapokuwa usingizini/usiku ilhali ung'amuzi hufanya kazi mtu akiwa yu macho/mchana

Swali (b)

Eleza mtazamo wa Freud kuhusu ung'amuzibwete.

Majibu

Mambo nayayopatikana katika ung'amuzibwete yana sifa hasi.

- Huficga/hubania mambo ambayo binadamu hawezi kuyasema (kadamnasi/wazi/peupe.)
- Hubania matamanio yasiyokubalika na jamii/makatazo ya jamii.

Powered By: www.manyamfranchise.com

- Hubania kauli zilizoharamishwa na miko ya jamii.

Swali (c)
Kwa mujibu wa Freud yaliyomo kwenye ung'amuzibwete hudhihirika vipi?

Majibu
Kwa ishara za ndoto
- Kwa mitelezo ya kauli
- Kwa ishara
- Kwa matumizi ya lugha ya kitamathali katika uandishi.

Swali (d)
Eleza tofauti ya mawazo kati ya Sigmund Freud na Carl Gustav Jung.

Majibu
Freud aliuangalia ung'amuzibwete kama jaa la mawazo mabaya, fikra na dhana hasi ilhali Jung aliwaza kuwili.
au
Jung alizuka na ung'amuzibwete binafsi na ung'amuzibwete jumuishi.
au
Jung aliongezea ung'amuzibwete jumuishi.

Swali (e)
Taja hoja inayowafungamanisha Jung na Freud.

Majibu
Ung'amuzibwete una uwezo wa kuathiri ung'amuzi na matendo ya binadamu ya king'amuzi.

Swali la pili: Ufupisho

MUHTASARI

Utaifa ni mshikamano wa hisia zinazowafungamanisha watu wanaoishi katika taifa moja. Taifa huundwa na watu wanaoishi katika nchi moja na ambao wanajitambua kisiasa kama watu wenye mwelekeo, mwono na hatima sawa. Utaifa umejengwa kwenye hisia za mapenzi kwa nchi na utambuzi wa kwamba rangi, cheo, hadhi, eneo, kabila au tofauti nyinginezo baina ya watu wanaoishi katika nchi moja si sababu ya kuwatenganisha.

Nchi moja huweza kuwa na watu wa makabila tofauti, wenye matabaka ya kila nui na mawazo ainati. Watu hao wanapotambua kuwa kuna sherisi nyingine inayowaunganisha kama fahari ya kuwa watu wa nchi hiyo, falsafa na imani sawa ambayo ishara yake kuu ni wimbo wa taifa na kuwa tofauti kati yao si muhimu huwa wamefikia kuunda taifa.

Mhimili mkuu wa utaifa ni uzalendo. Uzalendo ni mapenzi makubwa aliyo nayo mtu kwa nchi yake. Mapenzi haya ndiyo yanayoongoza matendo yake, matamanio yake, mawazo yake, itikadi yake, mwonoulimwengu wake na muhimu zaidi mkabala wake kuihusu nchi yake na hatima ya nchi yenyewe. Uzalendo ni nguzo muhimu sana ya taifa. Mzalendo hawezi kuyatenda mambo yanayoweza kuiletea nakama nchi yake.

Matendo ya mzalendo huangazwa na mwenge wa mema anayoitakia nchi au taifa lake. Hawezi kushiriki kwenye harakati na amali ambazo zinahujumu au kufumua mshikamano wa taifa zima au kutawaliwa na kitiba cha kutaka kujinufaisha yeye mwenyewe au jamii yake finyu. Matendo ya mzalendo wa kitaifa yanaongozwa na mwelekeo wa kuiboresha nchi yake. Swali linalomwongoza mtu huyo ni: nimeifanyia nini nchi yangu au taifa langu? Alhasili mtu anayeipenda nchi yake hawezi kuongozwa na umero wa kibinafsi tu wa kujilimbikia mali, utajiri au pesa. Yuko radhi kuhasirika kama mtu binafsi ili taifa au nchi yake inufaike.

Utaifa ni mche aali ambao unapaliliwa kwa uzalendo, kuepuka hawaa za nafsi, kusinywa na taasubi za kikabila na kuacha tamaa ya kujinufaisha. Hali hiyo inapofikiwa, hatima ya wanajamii wa taifa linalohusika huwa nzuri na mustakabali wao na wa vizazi vyao huwa wa matumaini makubwa.

Swali hili lilihitaji mtahiniwa asome kifungu na kusanisi hoja muhimu na kuzifanyia muhtsari bila kuacha mawazo muhimu wala kupoteza maana asili ya kifungu.
Mtahiniwa pia alihitaji stadi ya kutumia viunganishi vifaavyo ili kuleta mtiririko unaoridhisha.Watahiniwa wengi walilemewa katika upande wa kutumia viunganishi ili kutiririsha mawazo. Wengi waliinua sehemu ambazo hazikuwa na uhusiano wowote kihoja. Stadi ya kujieleza kwa mtiririko ufaao lazima ifundishwe.

(a) Dondoa sifa kuu za utaifa (maneno 40 – 50)

Powered By: www.manyamfranchise.com

(b) Kwa kutumia maneno kati ya 60-70, onyesha misingi ya kumtathmini mzalendo

4.5 MAPENDEKEZO

- Walimu waendelee kuwapa wanafunzi mazoezi ya maswali ya ufahamu na kusahihisha wakizingatia sarufi kwa sababu jambo hili linazingatiwa wakati wa kusahihisha mtihani wa kitaifa.

- Wanafunzi wasisitiziwe kwamba baadhi ya maswali ni ya stadi za juu kama matumizi na tathmini kwa hivyo maswali ambayo hayaonekani kuwa na majibu ya kuinua moja kwa moja huulizwa pia.

- Wanafunzi wapewe mazoezi ya muhtasari huku mtiririko ufaao ukisisitizwa mara kwa mara ndio wazoee kutumia viunganishi kutiririsha hoja katika kujibu maswali ya muhtasari.

*Masuala yote katika silabasi yafundishwe katika upana wake bila kubagua.

4.6 FASIHI (102/3)

Matokeo ya karatasi ya tatu (102/3) ya miaka ya 2006 hadi 2009.

Mwaka	**2006**	**2007**	**2008**	**2009**
Alama ya Wastani	48.48	43.49	31.17	32.72
Alama ya Tanganisho	14.63	13.12	13.64	13.11

Matokeo ya karatasi ya tatu (102/3 ya mwaka wa 2009 yameimarika kutoka alama ya wastani ya 31.17 mwaka wa 2008 hadi 32.72 mwaka wa 2009.

Tutachanganua swali la kwanza pekee katika karatasi hii kwa sababu lilikuwa la **lazima.** Pia ndilo lililoonekana kuwapa watahiniwa changamoto kidogo.

Swali hili lilikuwa ni la **muktadha** kutoka kwa riwaya ya **Utengano (S.A Mohamed).**
Watahiniwa hawakuweza kueleza muktadha wa maneno hayo vema; hali iliyopelekea watahiniwa wengi kushindwa kujibu sehemu zingine za swali hili.

Swali 1

"Katu asingajitia kibuibui na kutanga na njia. Lo, kachoshwa na shimiri za baruti anazoshindiliwa moyoni mwake."

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili.

Majibu

a) (i) Haya ni maelezo ya mwandishi kuhusu mawazo ya Selume;
(ii) Anahisi hana mume kwani Shoka amepuuza wajibu wake
(iii) Kama si wanawe, Selume hangejisumbua kutafuta chakula
(iv) Anahisi hana mume kwani shika amepuuza wajibu wake
(iii) Amemwachia jukumu la malezi na kutafuta riziki, kazi ya Shoka ni kudowea alichokitafuta Selume.

(b) Taja na ufafanue tamathali ya usemi iliyotumika katika dondoo hili.

Majibu

Sitiari/Jazanda:Mifano:Shimiri za baruti — alama 1
Kutaja — alama 1
Mfano — alama 1

Powered By: www.manyamfranchise.com

Maelezo:
→Matatizo ya ndoa na maisha ya Selume yanafananishwa na "Shimiri za baruti zanazoshindiliwa moyoni."
Matatizo hayoo yanamqumiza moyoni Alama 2

(1) Msemo: nahua
Mfano:Kutanga na njia
Maelezo:-hangaika akitafuta, enda huku na huko.

- Nidaa/siyahi Lo! katu. Kuonyesha hisia za kuchukizwa na mkondo wa ndoa yake.

(c) Eleza umuhimu wa kisa kinachorejelewa na dondoo.

Majibu

(C) (i) Kudhulumiwa kwa mwanamke katika ndoa mf .Selume na Shoka.
(ii) Kutowajibika kwa wanaume mf. Shoka
(iii) Wanawake kuendelea kubaki katika ndoa za matatizo kwa sababu ya watoto wao na kujitolea kuteketeza yaliyopuuzwa na waume zao.

(d) Kwa kurejelea matukio mengine katika riwaya ya Utengano, fafanua maudhui mawili yanayoashiriwa na dondoo hili.

Majibu

(d) 1. Asasi ya ndoa /unyumba – ya Maksuudi na Tamima na ya Maksuudi na Mwanasururu
(i) Matatizo kati ya mume na mke
(ii) Dhiki zinazowakumba wanawake katika ndoa
(iii) Tamima analazimika kutawa kwa amri ya mumewe Bw. Maksuudi
(iv) Hana ruhusa ya kutoka wala kumwalika mtu nyumbani.
(v) Analazimika kujifungua nyumbani licha ya ushauri wa madaktari kutokana na msimamo wa mumewe.
(vi) Bi Farashuu anapomsaidia kujifungua anacharazwa vibaya na mumewe na kufukuzwa nyumbani.
(vii) Ananyimwa uhuru wa kuwa na mwanawe mdogo anayeishia kufariki
(viii) Tabia ya Bw. Maksuudi inaishia kuivunja jamaa yao.
(ix) Bw. Maksuudi anamwacha mkewe na kuwafuata wanawake wengine kama Shoka anavyomwacha mkewe na kufuata wanawake wengine huko nje.
(x) Mwanamke ananyimwa uhuru wa kuishi kama kiumbe anayeweza kujiamulia.
(xi) Mwanamke hana uhuru wa kiuchumi → mf. Mwanasururu ananyimwa urithi wake.

2. (b) (i) Tabdila – mvuwa, kibaruwa
(ii) Lahaja – mte, kutipuza, mtilizi
(iii) Mazida – tisiya
(iv) Inkisari – ikajinamiya/lingiapo
(v) Kuboronga sarufi.
Kutaja 1, mfano 1 – zozote 2 x 2=4

(d) 1. Asasi ya ndoa /unyumba – ya Maksuudi na Tamima na ya Maksuudi na Mwanasururu
(xii) Matatizo kati ya mume na mke
(xiii) Dhiki zinazowakumba wanawake katika ndoa
(xiv) Tamima analazimika kutawa kwa amri ya mumewe Bw. Maksuudi
(xv) Hana ruhusa ya kutoka wala kumwalika mtu nyumbani.

Powered By: www.manyamfranchise.com

(xvi) Analazimika kujifungua nyumbani licha ya ushauri wa madaktari kutokana na msimamo wa mumewe.

(xvii) Bi Farashuu anapomsaidia kujifungua anacharazwa vibaya na mumewe na kufukuzwa nyumbani.

(xviii) Ananyimwa uhuru wa kuwa na mwanawe mdogo anayeishia kufariki

(xix) Tabia ya Bw. Maksuudi inaishia kuivunja jamaa yao.

(xx) Bw. Maksuudi anamwacha mkewe na kuwafuata wanawake wengine kama Shoka anavyomwacha mkewe na kufuata wanawake wengine huko nje.

(xxi) Mwanamke ananyimwa uhuru wa kuishi kama kiumbe anayeweza kujiamulia.

(xxii) Mwanamke hana uhuru wa kiuchumi → mf. Mwanasururu ananyimwa urithi wake.

4.7 MAPENDEKEZO

- Walimu wafundishe vitabu vilivyoteuliwa kwa ukamilifu wake huku wakizingatia ploti,wahusika,maudhui,mbinu na lugha.

- Wanafunzi wahimizwe kutambua masuala muhimu yanayojitokeza katika hadithi zote katika Mayai Waziri wa Maradhi na Hadithi Nyingine.

- Wanafunzi wawekewe misingi bora katika fasihi simulizi tangu kidato cha kwanza.

TANB. Ni dhahiri kwamba kwa jumla matokeo ya mtihani wa somo la Kiswahili yameimarika katika mwaka wa 2009 yakilinganishwa na mwaka wa 2008.Ni matarajio yetu kuwa walimu na wanafunzi watamakinika kujifaidi na mapendekezo tuliyoyatoa katika ripoti hii ili kuzidi kuboresha matokeo ya somo la Kiswahili katika siku za halafu.

Powered By: www.manyamfranchise.com